

Maswali

1. Mungu aliambia Waisraeli wakule nini kama chakula cha kipekee?
2. Walifanyia nini hiyo damu?
3. Usiku huo malaika alifanya nini Misri?
4. Malaika alifanya nini alipoona damu kwa mlango?
5. Wamisri waliambia Waisraeli wafanye nini?
6. Mbona Waisraeli waliogopa walipofika kwa Bahari ya Shamu?
7. Waisraeli walipona namna gani kutoka kwa Wamisri walipofika kwa Bahari ya Shamu?
8. Nini ilifanyika kwa Wamisri?
9. Waisraeli walipitia jangwani wakisafiri kuenda wapi?
10. Mungu aliwapa nini ya kuwaonyesha njia na kuwalinda?

Majibu

1. Waisraeli walikula nyama iliyookwa kama chakula cha kipekee.
2. Lazima wapake damu kwa milango yao.
3. Malaika aliua kila mzaliwa wa kwanza kwa kila nyumba ya Wamisri.
4. Malaika hakuua mzaliwa wa kwanza kwa nyumba iliyokuwa na damu.
5. Wamisri waliambia Waisraeli watoke Misri na waende.
6. Waisraeli walinaswa katikati ya Bahari ya Shamu na jeshi la magari ya Wamisri.
7. Mungu aliambia Musa anyoshe fimbo juu ya bahari na mawimbi yalirudi nyuma na kufanya njia kavu baharini.
8. Walizama maji ya bahari yaliporudi na kufunika.
9. Waisraeli walisafiri kurudi kwa nchi yenye Mungu aliwaahidi.
10. Mungu aliwapa nguzo ya wingu mchana iwaoongoze na nguzo ya moto usiku iwalinde.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 1 Mwaka wa 3



15 Kuvuka Bahari ya Shamu

Marejeo

Kutoka 12: 1 – 11 na 31 – 37; 14: 1 – 28

Kiini cha somo


Kuonyesha vile Mungu aliwatoa watu wake kutoka Misri na vile waliokoka kutoka kwa kifo kwa kutii amri za Mungu.

Maneno maalum

- 15.1 Mungu + ambia Musa + Waisraeli + chakula cha kipekee + oka mwana kondoo + paka mlangoni damu
- 15.2 Usiku + malaika Misri + ua wazaliwa wa kwanza + damu mlangoni + hakua + Wamisri waliogopa + waruhusu Waisraeli waende
- 15.3 Waisraeli + ondoka Misri + nguzo ya wingu + nguzo ya moto + Bahari ya Shamu + magari ya Wamisri + hakuna njia ya kuheba
- 15.4 Mungu alisaidia + fimbo ya Musa + njia baharini + fimbo ya Musa + maji yalirudi kwa kishindo
- 15.5 Wamisri + zama + Waisraeli + salama + jangwani

15.1 Musa alifurahi sana. Mungu alimwambia kwamba siku ifwatayo atawaongoza waondoke Misri. Kwa miezi kadha alikuwa akisihi Farao awaruhusu Waisraeli waende. Mungu alikuwa ametuma tauni nyingi kwa Wamisri kama adhabu, lakini Farao alikataa kuwaruhusu. Mwishowe sasa Mungu aliwaahidi kwamba kweli wataondoka Misri.

Mungu aliambia Waisraeli kwamba usiku huo lazima wote wale chakula kisicho cha kawaida. Lazima wale nyama ya mwana kondoo iliyookwa. Lazima wakule kama wamefunga vitu vyao vyote na wamevaa nguo tayari kusafiri. Kabla wakule chakula iliwalazimu kupaka damu kwa milango ya nyumba zao.



15.2 Waisraeli walifanya vile Mungu aliwaambia. Walioka mwana kondoo wa kukula. Wakizungusha baadhi ya damu ya kondoo kwenye milango yao. Usiku huo, malaika wa Mungu alitembea kwa kila nyumba na kuua mwana mzaliwa wa kwanza. Lakini malaika alipoona damu kwa mimo ya milango ya nyumba za Waisraeli, hakuua yeyote kwa hiyo nyumba.



Wakati wa usiku Wamisri waliona wanao wazaliwa wa kwanza wamekufa. Waliogopa wakijua kwamba hiyo ilikuwa adhabu kutoka kwa Mungu. Kwa hivyo waliambia Waisraeli kwamba waondoke na waende.


15.3 Waisraeli walitoka kwa nyumba zao haraka na kwenda kwa sababu walikuwa wako tayari.

Walitoka kwa nchi ya Misri wakiwa na furaha sana. Walisafiri siku mzima halafu usiku huo walipiga kambi kando ya jangwa. Mungu aliwatengenezea nguzo ya wingu ya kuwaonyesha njia. Aliwapa nguzo ya moto kuwalinda wakati wa usiku.

Baada ya kusafiri kwa siku chache, walipofika kwa ukingo wa Bahari ya Shamu, waliona wingu la vumbi nyuma yao kwa umbali. Bunde tu waliona jeshi la Wamisri na magari wanawafwata. Hawakuwa na namna ya kuwaheba. Bahari ilikuwa mbele yao na Wamisri wanawafwata nyuma. Waisraeli waliogopa sana.

15.4 Lakini Mungu alikuwa nao na aliwasaidia kuebuka. Mungu alimwambia Musa anyoshe fimbo yake juu ya bahari. Mawimbi yalirudi nyuma na kufanya kuta mbili mrefu ya maji, na njia kavu ilikuwa katikati ya bahari. Waisraeli waliharakisha hapo katikati hali wanasikia sauti ya magari ya Wamisri ikiwakaribia nyuma.

Hatimaye walivuka ng'ambo ya bahari. Magari ya Wamisri yaligwama ndani ya matope katikati ya bahari. Mungu aliambia Musa anyoshe fimbo yake tena juu ya bahari. Mawimbi ya maji yalirudi kwa kishindo tena pamoja na bahari ikawa vile ilikuwa.



15.5 Nini ilikuwa imefanyika kwa magari ya Wamisri? Magari yalikuwa yamegwama kwa matope. Wote walizama majini wakati maji yalirudi pamoja kwa haraka.



Kwa hivyo Waisraeli hawakuogopa tena. Waliendelea na safari yao ya jangwani wakienda kwa nchi yenye Mungu alikuwa amewaahidi. Mungu aliwaonyesha njia ya kuendea akitumia nguzo ya wingu na nguzo ya moto.